Q2

# TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA ZANZIBAR

## ROBO YA PILI (APRILI – JUNI), 2026

**24 Julai, 2026**

# TOLEO LA ROBO MWAKA LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA - ZANZIBAR KWA MWEZI WA APRILI- JUNI,2026

## UTANGULIZI

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu wa kuimarisha takwimu za jinsia nchini ikiwemo kukusanya, kuchambua na kutoa takwimu za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Toleo hili hutolewa kila baada ya miezi mitatu ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za udhalilishaji wa kijinsia hapa Zanzibar. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu 21.


## LENGO

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera nawatoa maamuzi

## MATUKIO YA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA YALIYORIPOTIWA POLISI APRILI-JUNI 2026


Jumla ya matukio 400 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa polisi kwa mwezi wa Aprili – Juni 2026 ambapo waathirika walikuwa 400. Waathirika wengi walikuwa watoto (waathirika 339 sawa na asilimia 84.8), wakifuatiwa na wanawake 53 (asilimia 13.2) na wanaume nane (8) sawa na asilimia 2.0. Miongoni mwa waathirika watoto 339, wasichana walikuwa 294 (asilimia 86.7) na wavulana walikuwa 45 sawa na asilimia 13.3 ya waathirika watoto wote.

**Kielelezo 1.1: Idadi ya Waathirika wa Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Aprili - Juni 2026**




Idadi ya Matukio ya kubaka yaliyoripotiwa yalikuwa 210, ambapo waathirika 194 walikuwa wasichana na 16 walikuwa wanawake. Tukio la kujaribu kubaka lilikuwa moja (1) ambapo mwathirika alikuwa mwanamke. Matukio ya kulawiti/kunajisi yalikuwa 31 ambapo waathirika 28 walikuwa wavulana na watatu (3) walikuwa wanaume. Matukio ya kuingilia kinyume na maumbile yalikuwa 31 ambapo waathirika wote walikuwa wasichana. Matukio ya kutorosha yalikuwa 35 ambapo waathirika 32 walikuwa wasichana na waathirika watatu (3) walikuwa wanawake. Matukio ya lugha ya matusi yalikuwa 32 ambapo waathirika 11 walikuwa wanawake, waathrika nane (8) wasichana, waathirika 12 walikuwa wavulana na mwathirika mmoja (1) mwanamme. Matukio ya shambulio la aibu/kukashifu yalikuwa 42 ambapo waathirika 12 walikuwa wanawake, waathirika 25 walikuwa wasichana, waathirika wanne (4) wavulana na mwathirika mmoja (1) alikuwa ni mwanamme. Matukio ya kutelekeza watoto yalikuwa matatu (3) ambapo waathirika wawili (2) walikuwa wasichana na mwathirika mmoja (1) ni mvulana. Tukio la uzinifu lilikuwa moja ambapo mwathirika ni mwanamke.Tukio la kuingilia maharimu lilikuwa moja (1) ambapo mwathirika alikuwa mwanamke. Matukio ya mauaji yalikuwa manne (4) ambapo waathirika watatu (3) walikuwa wanaume na mmoja (1) alikuwa mwanamke. Tukio la kutupa watoto lilikuwa moja (1) ambapo mwathirika alikuwa msichana, tukio la shambulio la mtoto lilikuwa moja (1) ambapo mwathirika alikuwa ni msichana, na matukio ya kumpa na kupokea ujauzito yalikuwa saba (7) ambapo waathirika wote walikuwa wanawake.

**Kielelezo 1.2 Idadi ya Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Aina ya Matukio Aprili –Juni , 2026**



Wilaya ya Magharibi 'A' imeripotiwa matukio mengi (matukio72) kwa robo ya pili ya Aprili hadi Juni, 2026 sawa na asilimia 18.0 ikifuatia Wilaya ya Magharibi 'B' ambayo imeripotiwa matukio 71 (asilimia 17.8). Wilaya ya Kusini imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio (matukio nane (8)) sawa na asilimia 2.0 ya matukio yote yaliyoripotiwa.

**Kielelezo 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Aprili – Juni, 2026**




Miongoni mwa waathirika watoto 339 waliofanyiwa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; Waliobakwa walikuwa wasichana 194, waliolawitiwa/kunajisi walikuwa wavulana 28, kuingilia kinyume na maumbile walikuwa wasichana 31, kutorosha walikuwa wasichana 32, shambulio la aibu/kukashifu walikuwa 29 ambapo wasichana walikuwa 25 na wavulana walikuwa wanne (4), lugha ya matusi walikuwa 20 ambapo wasichana walikuwa nane (8) na wavulana walikuwa 12, kutelekeza watoto walikuwa watatu(3) ambapo wasichana walikuwa wawili(2) na mvulana alikuwa mmoja (1), kutupa mtoto alikuwa msichana mmoja(1) na shambulio la mtoto alikuwa msichana mmoja(1).

**Jadweli 1.1: Idadi ya Matukio na Waathirika ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya Aprili -Juni, 2026**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti/Kunajisi | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | | Lugha ya Matusi | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Kutelekeza Mtoto | | Kutupa Watoto | | Shambulio la Mtoto | |
| | | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 23 | 15 | 2 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 18 | 13 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 34 | 27 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 5 | 3 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 55 | 29 | 2 | 6 | 3 | 0 | 2 | 6 | 5 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 57 | 20 | 5 | 9 | 11 | 0 | 3 | 3 | 5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 67 | 31 | 9 | 13 | 4 | 0 | 3 | 3 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 23 | 18 | 2 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 10 | 7 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 22 | 11 | 1 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 25 | 20 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **339** | **194** | **28** | **31** | **32** | **0** | **8** | **12** | **25** | **4** | **2** | **1** | **1** | **0** | **1** | **0** |

Miongoni mwa wanawake 53 ambao ni waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; waliobakwa walikuwa 16, Kujaribu kubaka alikuwa mmoja (1), Kutorosha walikuwa watatu (3), Lugha ya matusi walikuwa 11, Shambulio la aibu/Kukashifu walikuwa 12, Kuingilia maharimu alikuwa mmoja (1), mauaji alikuwa mmoja (1), Kumpa na kupokea ujauzito walikuwa saba (7) na uzinifu alikuwa mmoja (1).

**Jadweli 1.2: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya Aprili - Juni, 2026**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kujaribu Kubaka | Kutorosha | Lugha ya Matusi | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Kuingilia Maharimu | Mauaji | Kumpa na Kupokea Ujauzito | Uzinifu |
| Kaskazini 'A' | 4 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 1 |
| Kusini | 3 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 13 | 5 | 0 | 0 | 3 | 1 | 0 | 0 | 4 | 0 |
| Magharibi 'A' | 14 | 4 | 1 | 1 | 3 | 3 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Magharibi 'B' | 4 | 0 | 0 | 0 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 3 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 6 | 4 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| **Jumla** | **53** | **16** | **1** | **3** | **11** | **12** | **1** | **1** | **7** | **1** |

Kwa mwezi wa Aprili – Juni 2026, idadi ya waathirika wanaume walikuwa ni nane (8), waathirika watatu (3) wa tukio la kulawiti, mwathirika mmoja (1) wa tukio la Lugha ya matusi, mwathirika mmoja (1) tukio la shambulio la aibu na waathrika watatu (3) wa tukio la mauaji.

**Jadweli 1.3: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanaume kwa Wilaya Aprili – Juni, 2026**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kulawiti/Kunajisi | Lugha ya Matusi | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Mauaji | Kumpa na Kupokea Ujauzito | Wizi wa Watoto |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 3 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 3 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | | 0 |
| Chake Chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **8** | **3** | **1** | **1** | **3** | **0** | **0** |

Watoto wenye umri wa miaka 15-17 wameripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio (matukio 216) sawa na asilimia 63.7 ya matukio yote ya watoto yaliyoripotiwa ikifuatiwa na umri wa miaka 11-14 (matukio 78) sawa na asilimia 23.0. Matukio 27 sawa na asilimia 8.0 yaliripotiwa kwa umri wa miaka 6-10 na umri wa miaka 0-5, yaliripotiwa matukio 18 sawa na asilimia 5.3. Aidha matukio ya kubaka yanaonesha kuwa mengi zaidi katika umri wa miaka 15-17 (matukio 149) sawa na asilimia 76.8 kati ya matukio yote ya kubaka yalioripotiwa.

**Jadweli 1.4: Aina ya Waathirika ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto na Umri Aprili – Juni, 2026**


| Umri | 0-5 | | 6-10 | | 11-14 | | 15-17 | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Wasichana** | **Wavulana** |
| Kubaka | 1 | | 5 | | 39 | | 149 | | 194 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 4 | | 10 | | 11 | | 3 | | 28 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 2 | | 4 | | 9 | | 16 | | 31 | |
| Kutorosha | 0 | 0 | 1 | 0 | 7 | 0 | 24 | 0 | 32 | 0 |
| Lugha ya matusi | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 1 | 4 | 11 | 8 | 12 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 4 | 2 | 6 | 1 | 7 | 0 | 8 | 1 | 25 | 4 |
| Kutelekeza mtoto | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 |
| Kutupa Watoto | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Shambulio la mtoto | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| **Jumla ya Waathirika** | **11** | **7** | **16** | **11** | **66** | **12** | **201** | **15** | **294** | **45** |

**Jadweli 1.5 : Idadi ya Waathirika Wanawake na Wanaume wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, kwa Umri na Aina ya Matukio; Aprili -Juni 2026**

| Umri | 18-24 | | 25-35 | | 36-45 | | 46-64 | | 65+ | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **Wanawake** | **Wanaume** | **Wanawake** | **Wanaume** | **Wanawake** | **Wanaume** | **Wanawake** | **Wanaume** | **Wanawake** | **Wanaume** | **Wanawake** | **Wanaume** |
| Kubaka | 14 | | 2 | | 0 | | 0 | | 0 | | 16 | |
| Kujaribu Kubaka | 1 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 1 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 2 | | 0 | | 0 | | 1 | | 0 | | 3 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kutorosha | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 |
| Lugha ya matusi | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 | 11 | 1 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 7 | 0 | 5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 | 1 |
| Uzinifu | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kuingilia maharimu | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mauaji | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 3 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 | 0 |
| **Jumla** | **42** | **2** | **9** | **2** | **0** | **2** | **2** | **1** | **0** | **1** | **53** | **8** |


Matukio mengi (matukio 212) yametokea nyumbani kwa mtuhumiwa sawa na asilimia 53.0 ikifuatiwa na idadi ya matukio yaliyotokea majumba mabovu (matukio 58) sawa na asilimia 14.5 na vichakani (matukio 53) sawa na asilimia 13.3 ikilinganishwa na maeneo mengine yaliyoripotiwa kwa mwezi Aprili – Juni 2026.

**Kielelezo 1.4: Idadi ya Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Sehemu Yaliyotokea Aprili - Juni, 2026**



Wafanyaji wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia walioripotiwa mwezi wa Aprili – Juni 2026 walikuwa 400 kati yao 173 walikuwa wapenzi sawa na asilimia 43.3, watu wasiojulikana walikuwa 107 sawa na asilimia 26.8, Jirani walikuwa 100 sawa na asilimia 25.0, watu wengine walikuwa 13 sawa na asilimia 3.2, baba/mama mzazi walikuwa sita (6) sawa na asilimia 1.5 na mwalimu wa skuli alikuwa mmoja (1) sawa na asilimia 0.2.

**Kielelezo 1.5: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatiki na Udhalilishaji wa Kijinsia Aprili - Juni, 2026**



## MAJALADA YA MAKOSA YA UDHALILISHAJI YALIYOPOKELEWA AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA ZANZIBAR APRILI - JUNI, 2026

Jumla ya Majalada 147 yamepokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwezi wa Aprili - Juni, 2026 ambayo yalihusisha makosa 157.

Idadi kubwa ya makosa yaliyopokelewa yametokea Mkoa wa Mjini Magharibi (makosa 98) sawa na asilimia 62.4 ya makosa yote ikilinganishwa na mikoa mwengine.

**Jadweli 2.1: Idadi ya Majalada na Mkosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa/ Makao Makuu Aprili - Juni, 2026**

| Mkoa/Makao Makuu | Idadi ya Majalada | Idadi ya Makosa |
|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 13 | 15 |
| Kusini Unguja | 10 | 10 |
| Mjini Magharibi | 92 | 98 |
| Kaskazini Pemba | 16 | 17 |
| Kusini Pemba | 15 | 16 |
| Makao Makuu | 1 | 1 |
| **Jumla** | **147** | **157** |

Kati ya Majalada 147 ya Udhalilishaji yaliyoripotiwa mwezi wa Aprili - Juni, 2026, majalada 63 yameruhusiwa kwenda mahkamani, majalada 37 hayajatolea uamuzi, majalada 31 yamerudishwa Polisi kwa Upelelezi zaidi na majalada 16 yamependekezwa kufungwa.

**Jadweli 2.2 Majalada ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa na Hatua, Aprili – Juni, 2026**

| Mkoa/ Makao Makuu | Idadi ya Majalada | Yalioruhusiwa kwenda Mahakamani | Yaliopendekezwa Kufungwa | Yaliorudi Polisi kwa Upelelezi | Hayajatolewa Uamuzi |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 13 | 6 | 0 | 0 | 7 |
| Kusini Unguja | 10 | 7 | 0 | 1 | 2 |
| Mjini Magharibi | 92 | 29 | 10 | 26 | 27 |
| Kaskazini Pemba | 16 | 9 | 3 | 4 | 0 |
| Kusini Pemba | 15 | 12 | 3 | 0 | 0 |
| Mkao Makuu | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| **Jumla** | **147** | **63** | **16** | **31** | **37** |

Miongoni mwa makosa 157 ya udhalilishaji yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, makosa mengi zaidi yaliyojitokeza yanahusiana na kubaka (makosa 84) sawa na asilimia 53.5 ya makosa yote yaliyopokelewa.


**Jadweli 2.3: Idadi ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa, Aprili- Juni 2026**

| Mkoa | Jumla ya Makosa | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Shambulio la Aibu/ Kukashifu | Kumuingilia Mlemavu wa Akili | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kalawiti /Kunajisi | Kumuinglia Mlemavu wa akili | Kumpa na Kupokea Ujauzito | Uzinifu | Kujaribu Kubaka | Kutorosha |
| Kaskazini Unguja | 15 | 9 | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Kusini Unguja | 10 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Mjini Magharibi | 98 | 51 | 9 | 0 | 20 | 12 | 0 | 0 | 1 | 1 | 4 |
| Kaskazini Pemba | 17 | 11 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 3 |
| Kusini Pemba | 16 | 4 | 5 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 5 |
| Makao Makuu | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **157** | **84** | **16** | **1** | **21** | **16** | **1** | **1** | **1** | **1** | **15** |

## MASHAURI NA MAKOSA YA UDHALILISHAJI YALIYOFUNGULIWA KATIKA MAHKAMA ZA UDHALILISHAJI ZANZIBAR KWA MWEZI WA APRILI – JUNI 2026

Jumla ya mashauri 52 yamefunguliwa katika mahakama za udhalilishaji kwa mwezi wa Aprili - Juni, 2026, ambapo yamehusisha makosa 57. Mkoa wa Mjini Magharibi umeripotiwa kuwa na mashauri mengi yaliyofunguliwa ambayo ni mashauri 24 yaliyohusisha makosa 27 sawa na asilimia 46.2 ya mashauri yote ikilinganishwa na mikoa mengine.

**Kielelezo 3.1: Mashauri ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyofunguliwa kwa Mkoa Aprili - Juni, 2026**




Kati ya mashauri 52 yaliyofunguliwa katika Mahkama za udhalilishaji Zanzibar, mashauri 37 bado yanaendelea sawa na asilimia 71.2, mashauri sita (6) yametiwa hatiani sawa na asilimia 11.5 na mashajuri tisa(9) hayakuwa na hatia sawa na asilimia 17.3.

**Jadweli 3.1: Idadi ya Mashauri ya Ukatili na Udhalilishaji Zilizofunguliwa katika Mahkama na hatua zilizochukuliwa Aprili - Juni 2026**

| Aina ya Makosa | Zilizopokelewa | Zinazoendelea | Zilizotiwa Hatiani | | | | | Zisizo na Hatia | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kifungo | Faini | Fidia | Kifungo na fidia | Faini na fidia | Zilizoachiwa huru | Zilizondoshwa/Zilozofutwa |
| Kubaka | 22 | 15 | 0 | 1 | 0 | 0 | 3 | 2 | 1 |
| Kubaka na Kutorosha | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kubaka na kumuingilia kinyume na maumbile | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kubaka na kumuingilia kinyume na maumbile na kutorosha | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| K/kubaka na shambulio la aibu | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Jaribio la kubaka | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kulawiti | 5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 1 |
| Kujaribu k/maumbile | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kutorosha | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kutorosha na shambulio la aibu | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu | 4 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Udhalilishaji Mkubwa wa kingono | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kubaka mgonjwa wa akili | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **52** | **37** | **0** | **1** | **0** | **1** | **4** | **5** | **4** |

Jumla ya makosa 57 yaliyopokelewa katika Mahkama za udhalilishaji wa kijinsia, makosa mengi zaidi yaliyojitokeza yanahusiana na kubaka (makosa 24) sawa na asilimia 42.1 ya makosa yote yaliyopokelewa.

**Jadweli 3.2: Idadi ya Makosa ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia yaliyopokelewa Kimkoa kwa Aina ya Makosa Aprili -Juni, 2026**


| Mkoa | Kaskazini Unguja | Kusini Unguja | Mjini Magharibi | Kaskazini Pemba | Kusini Pemba | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kubaka | 4 | 2 | 9 | 4 | 5 | 24 |
| Kubaka kwa kundi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Jaribio la kubaka | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 0 | 1 | 3 | 0 | 0 | 4 |
| Kulawiti | 0 | 0 | 4 | 0 | 1 | 5 |
| Kujaribu kubaka na shambulio la Aibu | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 2 |
| Kutorosha na kubaka | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 |
| Shambulio la aibu | 0 | 0 | 2 | 1 | 3 | 6 |
| K/kumuingilia kinyume na maumbile | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 |
| Kubaka na kuingilia kinyume na maumbile | 0 | 2 | 4 | 0 | 0 | 6 |
| Kutorosha na sh/la aibu | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Kutorosha | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 |
| Kubaka mgonjwa wa akili | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 |
| Kutorosha na kubaka na k/maumbile | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 |
| **Jumla** | **4** | **5** | **27** | **8** | **13** | **57** |

## WANAFUNZI NA MAHABUSU WA MAKOSA YA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA WA CHUO CHA MAFUNZO

Jumla ya Wanafunzi wa makosa ya udhalilishaji waliopokelewa Chuo cha Mafunzo kwa Aprili – Juni, 2026 walikuwa 22 na Mahabusu walikuwa 59.


Wilaya ya Mjini imeripotiwa kupokea wanafunzi wengi (wanafunzi 6) sawa na asilimia 27.3 ukilinganisha na wilaya nyengine. Wilaya ya Magharibi 'A' imeripotiwa kuwa na mahabusu wengi zaidi (mahabusu 14) sawa na asilimia 23.7 ya mahabusu wote walioripotiwa kwa mwezi wa Aprili – Juni, 2026.

**Kielelezo 4.1: Idadi ya Wanafunzi na Mahabusu Waliopokelewa Chuo cha Mafunzo kwa Wilaya, Aprili - Juni, 2026**




Umri wa miaka 18-24 umeripotiwa kuwa na wanafunzi wengi zaidi (saba(7)) sawa na asilimia 31.8 kati ya wanafunzi wote walioripotiwa ikilinganishwa na umri mwengine. Aidha, kwa upande wa mahabusu umri unaoongoza ni miaka 25-35 (mahabusu 22) sawa asilimia 37.3 ya mahabusu wote walioripotiwa.

**Kielelezo 4.2: Idadi ya Wanafunzi na Mahabusu Waliopokelewa Chuo cha Mafunzo kwa Umri, Aprili – Juni 2026**



Wanafunzi wengi wamehukumiwa kutumikia kifungo cha mwaka 1 hadi 2 (wanafunzi 6) sawa na asilimia 38.5 ikilinganishwa na vifungo vyengine.

**Jadweli 4.3: Idadi ya Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo kwa Muda wa Vifungo na Aina ya Makosa, Aprili - Juni, 2026**

| Muda wa kutumikia kifungo Chuoni (Gerezani) | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu | Shambulio | Kuingilia Maharimu | |
| Chini ya miezi 3 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | **2** |
| Miezi 4-11 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mwaka 1-2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 4 | 0 | **6** |
| Miaka 3-5 | 0 | 0 | 0 | 1 | 4 | 0 | **5** |
| Miaka 6-10 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | **4** |
| Miaka 11+ | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | **4** |
| Kigungo cha maisha | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Hukumu ya Kifo | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **1** |
| **Jumla** | **5** | **1** | **4** | **2** | **9** | **1** | **22** |

**HITIMISHO**

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia, muda wa matukio yalipotokea na wafanyaji wa matukio. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu 21. Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

Jumla ya matukio 400 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa makao makuu ya Polisi kwa mwezi wa Aprili – Juni 2026 ambapo waathirika walikuwa 400. Waathirika wengi walikuwa watoto (waathirika 339 sawa na asilimia 84.8), wakifuatiwa na wanawake 53 (asilimia 13.2) na wanaume nane (8) sawa na asilimia 2.0.

Miongoni mwa waathirika watoto 339, wasichana walikuwa 294 (asilimia 86.7) na wavulana walikuwa 45 sawa na asilimia 13.3 ya waathirika watoto wote.

Wilaya ya Magharibi 'A' imeripotiwa matukio mengi(matukio72) sawa na asilimia 18.0 ikifuatia Wilaya ya Magharibi 'B' ambayo imeripotiwa matukio 71 (asilimia 17.8). Wilaya ya Kusini imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio(matukio nane (8)) sawa na asilimia 2.0 ya matukio yote yaliyoripotiwa.

Jumla ya Majalada 147 yamepokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwezi wa Aprili - Juni, 2026 ambayo yalihusisha makosa 157. Idadi kubwa ya makosa yaliyopokelewa yametokea Mkoa wa Mjini Magharibi (makosa 98) sawa na asilimia 62.4 ya makosa yote ikilinganishwa na mikoa mwengine.

Jumla ya mashauri 52 yamefunguliwa katika mahakama za udhalilishaji kwa mwezi wa Aprili - Juni, 2026, ambapo yamehusisha makosa 57.

Jumla ya Wanafunzi wa makosa ya udhalilishaji waliopokelewa Chuo cha Mafunzo kwa Aprili – Juni, 2026 walikuwa 22 na Mahabusu walikuwa 59.

**Kiambatanisho:**

**Jadweli 1: Idadi ya Matukio na Waathirika kwa Aina ya Waathirika Yalioripotiwa Polisi na Miezi, 2026**

| Robo Mwaka | Idadi ya Matukio | Jumla ya Waathirika | Idadi ya Waathirika | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Watoto | | Watu Wazima | |
| | | | Wasichana | Wavulana | Wanawake | Wanaume |
| Januari | 113 | 113 | 79 | 12 | 20 | 2 |
| Februari | 98 | 99 | 66 | 15 | 17 | 1 |
| Machi | 103 | 103 | 75 | 9 | 17 | 2 |
| **Januari-Machi** | **314** | **315** | **220** | **36** | **54** | **5** |
| Aprili | 129 | 129 | 93 | 15 | 19 | 2 |
| May | 128 | 128 | 96 | 13 | 17 | 2 |
| Juni | 143 | 143 | 105 | 17 | 17 | 4 |
| **Aprili- Juni** | **400** | **400** | **294** | **45** | **53** | **8** |
| Julai | | | | | | |
| Agosti | | | | | | |
| Septemba | | | | | | |
| **Julai-Septemba** | | | | | | |
| Oktoba | | | | | | |
| Novemba | | | | | | |
| Disemba | | | | | | |
| **Oktoba-Disemba** | | | | | | |
| **Januari-Disemba** | | | | | | |

**Jadweli 2: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika na Aina ya Matukio Aprili -Juni, 2026**

| Sehemu Zilotokezea | Nyumbani kwa Muathirika | | Nyumbani kwa Mtuhumiwa | | Nyumba za wageni/rafiki | | Sehemu za kazi | | Majumba mabovu | | Vichakani | | Vyombo vya Usafiri(Gari) | | Sehemu nyengine | | jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** | **W'ke** | **W'me** |
| Kubaka | 4 | | 125 | | 5 | | 1 | | 29 | | 40 | | 0 | | 6 | | 210 | |
| Kujaribu kubaka | 0 | | 1 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 1 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 1 | | 11 | | 0 | | 0 | | 11 | | 5 | | 0 | | 3 | | 31 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 0 | | 18 | | 0 | | 0 | | 11 | | 2 | | 0 | | 0 | | 31 | |
| Kutorosha | 1 | 0 | 24 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 5 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 35 | 0 |
| Lugha ya matusi | 11 | 9 | 5 | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 19 | 13 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 17 | 3 | 14 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 4 | 0 | 37 | 5 |
| Kutelekeza mtoto | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 |
| Kuingilia maharimu | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Uzinifu | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mauaji | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 1 | 3 |
| Kutupa Watoto | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| Shambulio la mtoto | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 0 | 0 | 5 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 | 0 |
| **Jumla** | **34** | **14** | **197** | **15** | **9** | **0** | **2** | **0** | **47** | **11** | **46** | **7** | **1** | **0** | **11** | **6** | **347** | **53** |

**Jadweli 3.0: Idadi ya Waaathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Yalioripotiwa Polisi kwa Wilaya Aprili - Juni, 2026**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kujaribu kubaka | Kulawiti/ Kunajisi | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | | Lugha ya matusi | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Kuteleke za Mtoto | | Kuingilia maharimu | | Mauaji | | Kutupa Watoto | | Shambulio la mtoto | | Kumpa na Kupokea ujauzito | | Uzinifu | |
| | | W'ke | W'ke | W'me | W'ke | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me |
| Kaskazini 'A' | 27 | 17 | 0 | 2 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 19 | 13 | 0 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 41 | 27 | 0 | 4 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 3 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kusini | 8 | 4 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 68 | 34 | 0 | 2 | 6 | 3 | 0 | 5 | 6 | 6 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 72 | 24 | 1 | 5 | 9 | 12 | 0 | 6 | 3 | 8 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 71 | 31 | 0 | 9 | 13 | 4 | 0 | 6 | 3 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 29 | 18 | 0 | 3 | 1 | 2 | 0 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 11 | 7 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 28 | 15 | 0 | 1 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 6 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 26 | 20 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **400** | **210** | **1** | **31** | **31** | **35** | **0** | **19** | **13** | **37** | **5** | **2** | **1** | **1** | **0** | **1** | **3** | **1** | **0** | **1** | **0** | **7** | **0** | **1** | **0** |

**Jadweli 4.0: Muda wa Matukio ya Udhalilishaji Yalioripotiwa Polisi Yalipotokea; Aprili -Juni, 2026**

| Muda Uliyotokea Matukio | 12:01 - 03:00 Asubuhi | | 03:01 - 6:00 Mchana | | 6:01 - 9:00 Jioni | | 9:01 - 12:00 Jioni | | 12:01 - 3:00 usiku | | 3:01 - 09:00 Usiku | | 6:01 - 09:00 Usiku | | 09:01 - 12:00 Asubuhi | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jinsi** | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me |
| Kubaka | 9 | | 18 | | 42 | | 45 | | 81 | | 12 | | 2 | | 1 | | 210 | |
| Kujaribu kubaka | 0 | | 0 | | 0 | | 0 | | 1 | | 0 | | 0 | | 0 | | 1 | |
| Kulawiti/Kunajisi | | 4 | | 2 | | 4 | | 7 | | 11 | | 3 | | 0 | | 0 | | 31 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 0 | | 0 | | 5 | | 10 | | 14 | | 2 | | 0 | | 0 | | 31 | |
| Kutorosha | 0 | 0 | 2 | 0 | 6 | 0 | 13 | 0 | 12 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 35 | 0 |
| Lugha ya matusi | 1 | 0 | 1 | 1 | 5 | 4 | 4 | 8 | 8 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 19 | 13 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 2 | 0 | 6 | 0 | 12 | 2 | 7 | 2 | 8 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 37 | 5 |
| Kutelekeza mtoto | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 |
| Uzinifu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kuingilia maharimu | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mauaji | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 3 |
| Kutupa Watoto | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Shambulio la mtoto | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kumpa na kupokea ujauzito | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 | 0 |
| **Jumla** | **14** | **6** | **30** | **3** | **73** | **12** | **80** | **17** | **129** | **12** | **18** | **3** | **2** | **0** | **1** | **0** | **347** | **53** |

**Jadweli 5: Idadi ya Wanafunzi Waliofanya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Aprili– Juni, 2026**

| Wilaya | Kubaka | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu | Shambulio | Kuingilia Maharimu | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | **3** |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | **1** |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mjini | 1 | 1 | 2 | 1 | 1 | 0 | **6** |
| Magharibi 'A' | 2 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | **5** |
| Magharibi 'B' | 2 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | **5** |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | **2** |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **Jumla** | **5** | **1** | **4** | **2** | **9** | **1** | **22** |

**Jadweli 6: Idadi ya Mahabusu Waliofanya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Aprili– Juni, 2026**

| Wilaya | Kubaka | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kulawiti | Kujaribu Kulawiti | Kutorosha | Shambulio la Aibu | Kukashifu | Shambulio | Kuingilia Maharimu | Kubaka Mgonjwa wa Akili | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini 'A' | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | **5** |
| Kaskazini 'B' | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | **2** |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | **4** |
| Kusini | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | **4** |
| Mjini | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | **5** |
| Magharibi 'A' | 2 | 2 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 5 | 0 | 1 | **14** |
| Magharibi 'B' | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 7 | 0 | 0 | **10** |
| Wete | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | **3** |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | **1** |
| Chake chake | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 1 | 0 | **6** |
| Mkoani | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | **5** |
| **Jumla** | **12** | **3** | **2** | **0** | **2** | **4** | **1** | **32** | **1** | **2** | **59** |

**Jadweli 7: Idadi ya Mashauri Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia yaliyopokelewa Kimkoa kwa Aina ya Makosa Aprili -Juni, 2026**

| Mkoa | Kaskazini Unguja | Kusini Unguja | Mjini Magharibi | Kaskazini Pemba | Kusini Pemba | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kubaka | 4 | 2 | 9 | 4 | 3 | 22 |
| Kubaka na kutorosha | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 |
| Kubaka na kumuingilia kinyume na maumbile | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 | 4 |
| Kubaka na kumuingilia Kinyume na maumbile na kutorosha | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 |
| K/kubaka na shambulio la aibu | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 |
| Jaribio la kubaka | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 0 | 1 | 3 | 0 | 0 | 4 |
| Kulawiti | 0 | 0 | 4 | 0 | 1 | 5 |
| Kujaribu k/maumbile | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 |
| Kutorosha | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 |
| Kutorosha na shambulio la aibu | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 |
| Shambulio la aibu | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 4 |
| Udhalishaji mkubwa wa kingono | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Kubaka mgonjwa wa akili | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 |
| **Jumla** | **4** | **5** | **24** | **8** | **11** | **52** |

## Zingatia Maelezo

Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Kitendochochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu, kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi auya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mke, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamke kuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa , Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake na watoto wa kike na ponografia (uenezaji wangono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na maadili kama vile ubakaji, kulawiti, kuingilia kinyume na kimaumbile nashambulio la aibu;

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hiiya mwaka 2004. Sheria hii imetungwapamoja na mambo mengine kuyafanya baadhi ya matendo kuwa makosa ya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenyeshehemu ya kumi na tatu (Section thirteen)ya sheria ya adhabu imejumuisha makosa mengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendovya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Sheria ya mwenendo wa Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyohaviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesi zinazohusiana na ukatili na udhalilishajiwa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wakijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadikifungo cha maisha.

**Kwa Ufafanuzi zaidi Tafadhali Wasiliana na:-**

**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**
Sanduku la Barua,2321,
Simu: +255242231869
Barua pepe: cgs@ocgs.go.tzWebsite:
http://www.ocgs.go.tz

**MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR**
Sanduku la Barua, 237,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.comNukushi:
024223136
**MMP, Zanzibar.**